EACON 2024

CO-ORGANIZERS

PATRONAGE SPONSOR SPONSOR

TGCL

# Maafikiano Ya Kongamano La Afrika Mashariki
## Tarehe 24-25 Juni 2024, Mogadishu Somalia

## Utangulizi

Kongamano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2024, iliyofanyika Mogadishu Somalia kuanzia tarehe 25 kwa uwepo wa Rais wa Shirika la Taifa la Somali, mheshimiwa Hassan Sheikh Mohamud, Naibu wa waziri mkuu wa shirikisho la taifa la Somalia mheshimiwa Sala Jama, mawaziri, baraza la biashara, sekta binafsi, mashirika ya asasi za kiraia, wasomi vijana, kina mama na wanahabari walioshirikishwa kwa mada kuu ya "Kutilia mkazo ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki."

**1.** Wanapongeza kutiwa kwa sahihi mkataba wa kukubalika kwa shirikisho la Taifa la Somalia kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Ikulu ya Entebee tarehe 15 Disemba 2023.

**2.** Wanaisifu pia mkutano wa kuweka mikakati ya kujumuisha shirikisho la taifa la Somalia kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika tarehe 12-21 Juni jijini Nairobi, Kenya.

**3.** Wanathibitisha tena kanuni za nguzo ya uwiano wa Afrika Mashariki Ajenda 2026, malengo ya maendeleo endelevu ya ajenda 2030, mkataba wa Umoja wa mataifa kuhusu mabadiliko ya hali ya anga na makubaliano ya Paris.

**4.** Wanapongeza pia shirikisho la taifa la Somalia kwa uamuzi wa kimkakati kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki na ufanisi wa makubaliano hayo yaliyo ya kihistoria hasa kwa kuangazia maendeleo ya sasa ya kushirikisha Jumuiya kwa jumla.

**5.** Wanatambua uzinduzi wa mpango wa mabadiliko ya taifa kuanzia mwaka wa 2025-2029 kama mkakati wa maendeleo endelevu, ustawi wa uchumi na mafanikio ya muda mrefu.

**6.** Wanatambua kushirikishwa na kuhusika kwa ufanisi wa taifa la Somalia katika COP28 na makubaliano ya UAE.

### Kwa hivyo tunatambua mambo yafuatayo kuwa Ajenda ya kutiliwa mkazo na kuchukuliwa hatua ya haraka:-

**1.** Twahimiza jamii ya Somali na washikadau wote kuchukua hatua kwa kuzingatia uwiano wa jumuiya katika sekta ya biashara, elimu, kijamii na kubalishana tamaduni zao.

**2.** Kusisitiza umuhimu wa kufanikisha biashara ya kanda na kuwekeza kwa kuondoa vikwazo vya biashara, kusawazisha desturi na utaratibu na kukuza njia za usafirishaji ili kuwezesha bidhaa kusafirishwa mufti kupita mipaka mbalimbali.

**3.** Kuhimiza wasomi wa Somalia kuipa kipaumbele elimu na kujenga ujuzi kwa kushirikiana na vyuo vikuu, taasisi za kiufundi na vituo vya mafunzo ya ufundi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuhakikisha wanapata elimu bora kwa wote hasa wanawake na vijana.

- Ili kufikia hili, shirikisho la taifa la Somalia kwa uratibu na baraza la mseto wa vyuo vikuu vya Afrika Mashariki kwa Ushirikiano na wizara ya elimu, utamaduni na elimu ya juu watawezesha ufadhili wa elimu wa wanarika 1000 wa Somali, kusoma katika vyuo vikuu mbalimbali vya Afrika Mashariki.
- Twasihi wizara ya elimu, utamaduni na elimu ya juu kujiunga na muungano wa ujuzi wa kidijitali na utafiti wa shirika la Afrika Mashariki.

**4.** Kutetea uhenzi wa mipango ya kubadilishana mila na tamaduni za kijamii ili kutia nguvu uelewano na ushirikiano miongoni mwa jamii zilizo na mila tofauti tofauti katika Afrika Mashariki kwa nia ya kupongeza na kusherekea mila hizo na kudumisha utangamano wa kanda.

**5.** Kusisitiza haja ya kuwa na mikakati bora ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya anga na kudumisha mazingira bora kwa kuhimiza mataifa husika kutekeleza sera inayoshabihiana na UNFCCC na makubaliano ya Paris pia kuwekeza matumizi ya nishati mbadala na zaraa endelevu ili kujenga hali ya anga thabiti.

**6.** Kuhimiza kufanikishwa kwa miundo ya afya ya umma na ushirikiano wa sekta ya afya hasa kwa kukabiliana na majanga na mambo ibuka yanayotishia afya ya umma kwa kugawana ujuzi na rasilimali miongoni mwa mataifa husika ya Afrika Mashariki.

**7.** Kuonyesha umuhimu wa amani na usalama katika kanda la Afrika Mashariki na kuhimiza ushirikiano kwa kukubaliana na migogoro, ugaidi na uhalifu wa kimataifa kwa kushirikiana na kugawana habari muhimu.

**8.** Kuhimiza sekta binafsi na baraza la biashara kujihusisha kikamilifu katika kuendesha ukuaji wa uchumi na nafasi za kazi, kuwezesha uvumbuzi na kuunga mkono ujasiria mali san asana miongoni mwa vijana na wanawake.

**9.** Kutambua nafasi ya asasi za kiraia katika kuendeleza uwiano na maendeleo ya ukanda na kutilia mkazo kuhusishwa kwao katika kutunga sera mbalimbali na utekelezaji.

**10.** Kujitolea kwa uwazi na uwajibikaji wa utawala kwa kuhakikisha kuwa sheria inazingatiwa na kila taifa mwanachama, sera za kidemokrasia na kuheshimu haki za kibinadamu.

**11.** Kuahidi kutia nguvu serikali ya Somalia na sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuweza kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ajenda zilizokabiliwa na kuhakikisha kuna matokeo ya kutamaniwa kwa wakati mwafaka.

**12.** Kusihi washirika wa kimataifa na wafadhili kuunga mkono mipango ya Somalia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutambua uwezo wa ukanda kwa maendeleo endelevu na umuhimu wake kimkakati katika kukuza ustawi wa kikanda na dunia nzima.

**Kimepitishwa Mogadishu, Somalia tarehe 25 Juni 2024.**

**MWISHO**

Get In Touch
www.eaccon.com
info@eaccon.com
Mogadishu, Somalia